

التَّطْيِيرُ بِشَهْرِ صَفَرٍ

KUKOROFIKA NA MWEZI WA SAFAR

[MFUNGO TANO]

Amesema Ibn Rajab رَحْمَةُ اللَّهِ

[Ama kuhusisha Ukorofi (bahati mbaya) katika wakati fulani pasi na wakati mwingine, kama vile mwezi wa Safar (mfungo tano) au mwezi mwingine, jambo hilo si sahihi. Na hakika nyakati zote zimeumbwa na Allaah Ta'alaah, na ndani yake hutokea matendo ya Binadamu. Basi wakati wowote ambao muislamu atajishughulisha na kumtii Allaah, huo ni wakati wenye Baraka kwake, na wakati wowote ambao mja atajishughulisha na kumuasi Allaah, huo ni wakati wa Ukorofi (bahati mbaya) kwake. Hakika ya Ukorofi ni kumuasi Allaah]⁽¹⁾.

Mwandishi

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

¹- Tazama kitabu: [Latwaaiful Ma'ari] (Uk. 75).

Kila sifa njema anastahiki Allaah, Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Baada ya hayo:

Siku moja iliyopita nilituma Makala kwa ajili ya kuelezea jambo la Tatwayyur (Kukorofika), hasa hasa katika mwezi huu wa Safar (mfungo tano). Lakini nimeshuriwa na baadhi ya ndugu zangu wabora (Allaah awhifadhi) ya kwamba nitoe ufafanuzi kuhusiana na neno (kukorofika), kwani huenda watu wengi wasielewa nini makusudioa ya neno hilo.

- Asili ya neno At-Tatwayyur ni neno la kiarabu (التَّطَيُّرُ), maana yake ni mtu kujikalifisha kujua kheri au shari kwa kuzingatia mwelekeo wa ndege, baadae likatumika neno hilo kwa kitu chochote ambacho mtu atatumia kujibashiria kheri au kujitia mikosi, kama vile siku au mwezi fulani, au mnyama fulani aliyemuona n.k.

Mfano: Alikuwa mtu anapotaka kusafiri anatoka nje ya nyumba halafu anamrusa ndege ili aangalie mwelekeo wake; akielekea upande wa kulia hiyo ni ishara ya kheri katika safari yake, kwa hiyo ataenda safari yake hiyo kwa kuzingatia ule mwelekeo wa ndege, lakini akielekea upande wa kushoto hiyo ni ishara mbaya (ni shari) katika safari yake, kwa maana hatoenda safari yake, kadhalika wakitumia kama hivyo kwenye mambo yao mengine; kama vile harusi, biashara n.k. hii ndio ilikuwa kawaida ya waarabu wengi kabla ya kuja Uislamu, na baada ya Uislamu kuna waliobaki na itikadi katika washirikina, na hata katika miji yetu wapo ndugu zetu waislamu wanaoamini mambo hayo. Kwa hiyo tumejua kwamba neno hili lina pande mbili; lina maana ya kujitia mikosi, nuksi, uchuro, ukorofi n.k. na pia hutumika kwa maana ya kujibashiria kheri, Baraka n.k. Na Mtume ﷺ akipenda kujibashiria kheri na ametukataza sisi kujitia mikosi na nuksi si kwa ndege wala mwezi wa Safar (mfungo tano) wala kitu chochote, na wala mtu asiache kutimiza makusudio yake kwa ishara fulani aliyoiona akidhani kwamba ni nuksi.

Wabillaahi Ttaufiq

Abu Halima Arafat. 10/Safar/1444h-6/8/2022m.